## Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina

# Mwongozo wa Wazazi




Mwongozo wa Huduma za Mpango wa Watoto Wachanga Zinazotolewa Kwako na kwa Mtoto Wako

## Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina Ni Nini?

Kila familia inataka mtoto wao akue na kujifunza kwa kiwango kamili cha uwezo wake. Hali ya kuwa na wasiwasi kuhusu maendeleo ya mtoto wenu inaweza kuwa jambo geni kwenu kama familia na kuonekana kuwa ngumu. Kutakuwa na watu wageni wa kukutana nao na maneno na istilahi mpya za kuelewa, lakini hauko peke yako. Ni muhimu kukumbuka kuwa kuna misaada inayopatikana ili kusaidia kurahisisha hali hii kwa mtoto na familia yako. Ni hiari yako kushiriki katika Mpango wa Watoto Wachanga. Wazazi wanaweza kuchagua kuendelea kushiriki kulingana na muda wao, kukomesha utathmini wa hali ya kustahiki kushiriki au kujiondoa kwenye mpango wakati wowote.

Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEA, Individuals with Disabilities Education Act) ni sheria ya elimu ya nchi inayosaidia kuimarisha umuhimu wa maendeleo ya mapema na kujifunza kwa watoto wadogo. Sehemu ya C ya sheria ya IDEA huhakikisha kuwa misaada na huduma za suluhu za mapema zinapatikana kwa watoto wachanga wenye ulemavu, kuanzia wanapozaliwa hadi wenye umri wa miaka mitatu na familia zao. Katika North Carolina, mfumo wa Sehemu ya C wa sheria ya IDEA unaitwa Mpango wa Watoto Wachanga. Mpango wa Watoto Wachanga ni mfumo wa misaada iliyopangwa ya familia ya kukusaidia utimize mahitaji ya maendeleo ya mtoto wako. Taasisi kuu Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina ni Kitengo cha Suluhu za Mapema cha Sekta ya Ustawi wa Watoto na Familia cha North Carolina. Katika jamii yako, Mashirika ya Huduma za Maendeleo ya Watoto (CDSAs, Children’s Developmental Services Agencies) hutoa, kusimamia na kufuatilia mipango na shughuli za Mpango wa Watoto Wachanga. Kuna CDSA 16 katika jimbo nzima zinazowezesha kupata huduma za Mpango wa Watoto Wachanga. Mtandao huu wa CDSA unahudumia kaunti 100 za North Carolina katika maeneo ya huduma ya kaunti moja au kaunti nyingi.




*Matumaini na ndoto za watoto zipo mioyoni mwa familia zao.*
*Familia huwekeza kupitia muda, hisia na fedha.*
*Suluhu za Mapema husaidia familia kufanikisha ndoto hizo.*

## Kanuni za Mpango wa Watoto Wachanga ni zipi?

Familia zinajua na kuelewa mahitaji ya watoto wao vizuri kuliko mtu mwingine yeyote. Mpango wa Watoto Wachanga unathamini na kuzingatia jukumu la familia kama ufunguo wa ufanisi wa suluhu za mapema. Kwa hivyo, familia inahitaji kushirikiana kwa ukweli na washirika wa timu ya suluhu za mapema. Watoto husaidiwa vizuri ndani ya familia, na familia husaidiwa vizuri ndani ya jamii. Shughuli za suluhu zinazoendana na ratiba yako ya kila siku zinaweza kukupa matokeo unayotaka kwa mtoto na familia yako.

- *Mtoto anapaswa kuchukuliwa kama mtoto kwanza, badala ya kuchukuliwa kama mtoto mwenye “mahitaji maalum”.*
- *Jinsi ambavyo watoto na familia hukua na kuendelea, misaada na huduma pia hubadilika ili kutimiza mahitaji na machaguo.*
- *Suluhu ya mapema huwa na manufaa zaidi wakati familia zinasaidiwa katika kutimiza mahitaji ya watoto wao ndani ya muktadha wa shughuli na ratiba za kawaida za familia.*
- *Watoto wenye mahitaji maalum huhudumiwa vizuri katika mazingira yanayotumiwa na watoto wote.*
- *Imani na maadili ya familia ni muhimu na vinapaswa kuheshimika, vilevile msingi wa utamaduni (dini, kabila na asili) wa familia.*
- *Ushirikiano kati ya familia na watoa huduma ni muhimu kwa kupanga misaada na huduma za suluhu za mapema.*

## Ni Nani Anayestahiki Kupokea Huduma za Mpango wa Watoto Wachanga?

Mtoto na familia yako inaweza kupokea misaada na huduma za Mpango wa Watoto Wachanga ikiwa mtoto wako hajafikisha umri wa miaka mitatu na anatimiza vigezo vya mojawapo ya aina mbili za kustahiki kushiriki vilivyoelezwa hapa chini.

### *Aina ya I. Kuchelewa Kukua*

Hatua ambazo watoto wachanga na watoto hupitia zinajumuisha ujuzi mbalimbali, kama vile kutembea na kuzungumza. Ujuzi huu au hatua za ukuaji, kwa kawaida hutokea akifikisha umri fulani. Watoto wengi hukuza ujuzi kwa mpangilio unaotabirika. Hutambaa kabla ya kutembea, na huashiria kwa mkono kabla ya kutumia maneno kukuambia wanachotaka. Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kila mtoto hukua katika mtindo wake binafsi kwa wakati wake.

Mpango wa Watoto Wachanga huchukulia kuwa mtoto ana tatizo la kuchelewa kukua ikiwa mtoto huyo ameachwa nyuma zaidi na watoto wengine wa umri kama wake katika sehemu moja au zaidi zifuatazo:

- *Ukuaji wa Kiakili - ujuzi wa kufikiria na kujifunza*
- *Ukuaji wa Kimwili - kutembea, kuona, kusikia na afya*
- *Ukuaji wa Mawasiliano - kuelewa na kutumia sauti, ishara na maneno*
- *Ukuaji wa Kijamii na Kihisia - kujibu na kukuza mahusiano na watu*
- *Ukuaji wa Mazoea - kujitunza anapofanya mambo kama vile kula chakula au kuvaa*

Maendeleo ya mtoto wako yatatathminiwa kupitia njia mbalimbali ikijumuisha uchunguzi, ripoti ya mzazi na tathmini na ukadiriaji unaofanywa na wataalamu wa masuala ya ukuaji. Tathmini na ukadiriaji hubinafsishwa ili kushughulikia mahitaji na changamoto za kipekee za mtoto na familia yako.

### *Aina ya II: Tatizo Lililobainishwa*

Mtoto huchukuliwa kuwa ana tatizo lililobainishwa ikiwa ana tatizo lililotambuliwa la kimwili au kiakili ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha kuchelewa kukua. Mifano inajumuisha kasoro fulani za kijenetiki, kasoro za kinyurolojia, kuchelewa kukua zaidi, tatizo la kuona, kutoweza kusikia au ugonjwa wa akili.

*(Maelezo ya hapo juu ni mihtasari na si ufafanuzi wote wa aina za kustahiki kushiriki. Unaweza kupata maelezo zaidi kwa kumwuliza Mratibu wako wa Huduma ya Suluhu za Mapema katika CDSA iliyo karibu nawe au kwa kutembelea [www.ncdhhs.gov/itp-beearly](http://www.ncdhhs.gov/itp-beearly).)*



## Hali ya Mtoto Wangu ya Kustahiki Kushiriki Hubainishwaje?

Mtoto wako anapoelekezwa kwa mpango wa NC ITP, hali ya kustahiki kushiriki inaweza kubainishwa kwa njia mbili:

1. Rekodi za matibabu au rekodi zingine za mtoto zinaweza kutumika kubainisha ikiwa anastahiki kushiriki (bila kumtathmini mtoto) ikiwa rekodi hizo zinaonyesha kuwa mtoto wako ana tatizo la kuchelewa kukua au tatizo lililobainishwa linaloweza kutimiza vigezo vya kustahiki kushiriki vya jimbo.
2. Ikiwa hali ya kustahiki kushiriki kwa mtoto wako haiwezi kubainishwa kupitia ukaguzi wa rekodi za matibabu au rekodi zingine, utathmini utafanywa ili kubainisha ikiwa mtoto wako anastahiki kushiriki katika mpango huu.

Tathmini hufanywa na mfanyakazi mwenye ujuzi na inajumuisha kuhusishwa kwa taaluma au sekta mbili au zaidi tofauti. Katika kufanya utathmini, utaratibu mmoja hauwezi kutumika kubainisha hali ya mtoto ya kustahiki kushiriki katika mpango. Kwa hivyo, utathmini wa mtoto wako utajumuisha yafuatayo:

- Matumizi ya zana ya utathmini.
- Kumhoji mzazi/wazazi ili kupata historia ya matibabu na maendeleo ya mtoto.
- Kutambua kiwango cha utendaji cha mtoto wako katika sehemu za ukuaji za utambuzi, mawasiliano, kijamii na kihisia, mazoea, na ukuaji wa mwili ambao unajumuisha kuona na kusikia.
- Kukusanya maelezo kutoka kwa vyanzo vingine kama vile walezi wengine na watoa huduma za matibabu, ikiwa inahitajika, ili kuelewa kabisa uwezo na mahitaji ya kipekee ya mtoto wako, na kupitia rekodi za matibabu, elimu au rekodi zingine.

Ukadiriaji wa mtoto na ukadiriaji unaoelekezwa na familia hufanyika kwa watoto wote wanaostahiki kabla ya kubuniwa kwa Mpango wa Huduma Binafsi ya Familia (IFSP, Individualized Family Service Plan). Kuna maelezo zaidi kuhusu mpango wa IFSP baadaye katika kijitabu hiki. Ukadiriaji huu hufanywa ili kutambua uwezo na mahitaji ya kipekee ya mtoto wako na huduma za suluhu za mapema zinazofaa ili kutimiza mahitaji hayo na rasilimali, vipaumbele na changamoto za familia yako kuhusiana na kuimarisha maendeleo ya mtoto wako.

## Mratibu wa Huduma za Suluhu za Mapema Ni Nani?

Mratibu wa Huduma za Suluhu za Mapema ni mtu wa msingi unayewasiliana naye katika Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina. Mratibu huyo atashirikiana nawe ili kutafuta misaada na huduma za kutimiza mahitaji ya mtoto na familia yako. Familia nyingi huanza kushirikiana na Mratibu wa Huduma za Suluhu za Mapema mara tu watoto wao wanapoelekezwa katika Mpango wa Watoto Wachanga. Sheria za nchi na jimbo zinahitaji watoto na familia zinazohudumiwa na Mpango wa Watoto Wachanga ziwe na Mratibu wa Huduma za Suluhu za Mapema.

## Mratibu wako wa Huduma za Suluhu za Mapema Anaweza Kukusaidia:

- *Uelewe haki zako chini ya Mpango wa Watoto Wachanga wa NC*
- *Utambue mahitaji ya mtoto wako, chaguo za misaada na huduma unazotaka na njia za kupata misaada na huduma hizo.*
- *Upate misaada na huduma zilizoelezwa katika Mpango wa Huduma Binafsi ya Familia (IFSP) wa familia yako na kuhakikisha utoaji na ubora wa huduma hizo.*
- *Upate majibu ya maswali uliyo nayo kuhusu mtoto wako.*
- *Uzungumze na wataalamu wengine wanaoshirikiana na mtoto na familia yako.*
- *Uamue misaada na maelezo unayotaka, kiasi unachotaka na jinsi unavyotaka kupokea.*
- *Upate nyenzo ambazo huenda zikasaidia mtoto na familia yako.*
- *Upange wakati ambapo mambo yanapaswa kufanywa na uamue anayepaswa kuyafanya.*
- *Upangie mabadiliko ya huduma kwa kuzungumza kuhusu chaguo, kutembelea mipango mipya na kuweka mipango ya kuandaa kila mtu kwa mabadiliko hayo, ikijumuisha mpango wa mipito ya huduma wakati ambapo mtoto wako atafikisha umri wa miaka mitatu.*
- *Kusuluhisha migogoro yoyote na timu yako ya suluhu za mapema kuhusu mambo kama vile hali ya kustahiki kupokea huduma, aina za huduma na ada za huduma.*

## *Mpango wa Huduma Binafsi ya Familia (IFSP, Individualized Family Service Plan] Ni Nini)?*

Mpango wa Huduma Binafsi ya Familia au IFSP, ni mpango wa familia yako ulioandikiwa Mpango wa Watoto Wachanga. Unafafanua jinsi wewe na timu yako ya suluhu za mapema mtakavyoshirikiana ili kushughulikia mahitaji yaliyotambuliwa ya mtoto na familia yako. Mpango wa IFSP unahusu familia. Hii inamaanisha kuwa utakuwa mshirika mkuu na mwamuzi muhimu katika mpango wa IFSP.

Mpango wa IFSP unabuniwa kulingana na maelezo ya utathmini wa mtoto wako na kutokana na changamoto, rasilimali na vipaumbele unavyotambua. Kama vile ramani ya barabara au mpango wa usafiri, mpango wa IFSP huonyesha unakoelekea (malengo au matokeo ya mtoto na familia), jinsi na wakati utakapofika huko (huduma na muda unaokadiriwa), na atakayeandama nawe ili kukusaidia (watoa huduma, familia, marafiki, na/au misaada mingine ya jamii).

Mratibu wako wa Huduma za Suluhu za Mapema ana wajibu wa kukufafanulia mpango wa IFSP. Atahakikisha kuwa mpango wa IFSP umeandikwa na atajibu maswali yoyote uliyo nayo.

Saini yako unayotia kwenye mpango wa IFSP inaonyesha kushiriki kwako na kukubaliana na mpango huo. Hata hivyo, ikiwa hukubaliani na mpango wote au sehemu ya mpango wa IFSP, una haki ya kueleza wasiwasi wako na kuomba ufanyiwe mabadiliko. Unaweza kukubali au kukataa huduma yoyote au zote unazopendekezewa. Unaweza kukomesha huduma wakati wowote unaopenda. Lazima upewe nakala ya mpango wa IFSP baada ya kumaliza kubuniwa na kutiwa saini.

Mpango wa IFSP ulioandikwa hukaguliwa baada ya kila miezi sita. Hata hivyo, mahitaji na nyenzo zako huenda zikabadilika mara kwa mara. Unaweza kuomba mpango wako wa IFSP usasishwe au ukaguliwe wakati wowote.

## Ni Nani Atakayehusika Katika Kubuni Mpango wa IFSP wa Familia Yetu?

Wewe na timu yako ya mpango wa IFSP mtashirikiana ili kubuni mpango wenu na kukubaliana kuhusu huduma na misaada yoyote itakayotimiza vizuri mahitaji ya mtoto wako na kuendana na ratiba za familia yako. Watu ambao ni lazima wahusishwe ni:

- *Wewe (mzazi mmoja au wote wawili, walezi, walezi au wa kupanga)*
- *Mratibu wako wa Huduma za Suluhu za Mapema*
- *Washirika wa timu yako ya utathmini*
- *Iwapo inafaa, watoa huduma za suluhu za mapema, wako au wa mtoto wako*

*Unaweza kualika watu wengine katika timu yako ya mpango wa IFSP, kama vile wanafamilia wengine au wakili au mtu wa nje ya familia yako.*

## Ni Huduma Gani Zinazopatikana kwa Ajili ya Mtoto na Familia Yangu?

Aina mbalimbali za misaada na huduma zinapatikana kupitia Mpango wa Watoto Wachanga. Baadhi yake ni huduma zinazohitajika. Hii inamaanisha kuwa Mpango wa Watoto Wachanga lazima uzitoe ikiwa zimejumuishwa katika mpango wako wa IFSP.

Huduma zinazohitajika zinajumuisha:

Huduma na Vifaa vya Teknolojia Saidizi
Huduma za Kusikia
Mafunzo ya Familia, Ushauri na Ziara za Nyumbani
Huduma za Afya
Huduma za Matibabu
Huduma za Uuguzi
Huduma za Lishe
Tiba ya Matatizo ya Kikazi
Tiba ya Mwendo
Huduma za Kisaikolojia
Huduma za Uratibu wa Huduma
Lugha ya Ishara na Lugha ya Vidokezo
Huduma za Mapumziko
Huduma za Jamii
Maelekezo Maalum/Huduma za Urekebishaji za Jamii (CBRS, Community Based Rehabilitation Services)
Huduma za Tiba ya Lugha ya Matamshi
Usafiri na Gharama Husika
Huduma za Kuona

Huduma zingine huenda zikawekwa kwenye mpango wako wa IFSP lakini hazihitajiki kisheria kutolewa na Mpango wa Watoto Wachanga. Mratibu wako wa Huduma za Suluhu za Mapema anaweza kukusaidia kutafuta na kupata huduma hizi. Mifano ya huduma zingine ambazo wakati mwingine zinapendekezwa ni:

- *Malezi ya Mtoto*
- *Ziara za Mtoto Mwenye Afya*
- *Ushauri wa Kijenetiki*
- *Mpango wa Wanawake na Watoto (WIC, Women, Infants, and Children)*

## Haki za Familia Yako


Tafadhali rejelea Mwongozo wa “Taarifa ya Haki za Mtoto na Familia”, ambao unaeleza haki zako, pamoja na kufafanua kuwa una haki ya kufahamishwa kuhusu kanuni mahususi za ulinzi chini ya Mpango wa Watoto Wachanga wa NC. Kanuni hizi za ulinzi ni kuwa utakuwa mwamuzi mkuu na mashirika ya suluhu za mapema yatafuata taratibu zinazohitajika.

## Mpango wa Mabadiliko Ni Nini?

Familia yako huenda ikaridhika na misaada na huduma ambazo wewe na mtoto wako mnapokea kupitia Mpango wa Watoto Wachanga. Mtoto wako anapokaribia kufikisha umri wa miaka mitatu, huenda ikawa vigumu kufikiria kuhusu mipito. Mpango wa mipito ni utaratibu unaoendelea na hufanyika kwa njia nyingi tofauti, kama vile kupitia mazungumzo yasiyo rasmi na mikutano iliyopangwa. Mratibu wako wa Huduma ya Suluhu ya Mapema atakuelekeza katika utaratibu wa kubuni mpango wa mipito na ataongoza kubuniwa kwa Mpango wa Mpito ulioandikwa wa kujumuishwa katika mpango wako wa IFSP.

*Shughuli za kubuni mpango wa mpito zinajumuisha:*

- *Mazungumzo na ukusanyaji wa maelezo kuhusu chaguo za uwekaji wa baadaye, huduma na misaada katika jamii yako.*
- *Usaidizi wa kukuandaa wewe na mtoto wako kwa mabadiliko ya huduma.*
- *Kutoa maelezo kuhusu mtoto wako (kama vile ripoti za utathmini na ukadiriaji, na mipango ya IFSP), kwa idhini yako ya maandishi, kwa watoa huduma wengine.*



# Utaratibu wa Mpango wa Watoto Wachanga

Huu ni muhtasari wa hatua ambazo huenda familia yako ikafuata inaposhiriki katika Mpango wa Watoto Wachanga.

**Hatua za Kwanza: Kuanza**

### 1. Uelekezaji

- **Mtu yeyote, ikijumuisha mzazi,** aliye na wasiwasi kuhusu mtoto wake anaweza kumwelekeza kwa Mpango wa Watoto Wachanga.
- Uelekezaji unaweza kufanywa kwa simu, faksi, kwa maandishi au ana kwa ana kwa CDSA iliyo karibu.
- Ombi la uelekezaji linapopokewa, Mratibu wa Huduma za Suluhu za Mapema atateuliwa ili kuisaidia familia yako.

### 2. Mikutano ya Mwanzo

- Wakati wa mikutano yako ya mwanzo na mratibu wa huduma na mfanyakazi mwingine wa CDSA, utaulizwa kuhusu mtoto wako, maendeleo yake na historia ya matibabu.
- Mikutano hii ya mwanzo itatusaidia tuelewe wasiwasi na vipaumbele vyenu kama familia, uwezo wa sasa wa mtoto wako na sehemu zinazohitaji kuboreshwa, pamoja na mafanikio na changamoto ambazo huenda ukapata katika shughuli za kila siku.

### 3. Tathmini na Ukadiriaji

- Ili kubainisha ikiwa mtoto wako anastahili kupokea huduma za Mpango wa Watoto Wachanga, utathmini wa uwezo wa sasa wa mtoto wako unaweza kufanywa.
- Maelezo yanayokusanywa kupitia ukadiriaji yatatuonyesha uwezo wa mtoto wako na sehemu zozote za ukuaji zinazoweza kunufaika kutokana na msaada wa suluhu za mapema.

**Hatua Zinazofuata: Huduma**

### 4. Mpango wa Huduma Binafsi ya Familia (IFSP, Individualized Family Service Plan)

- Baada ya mtoto wako kubainishwa kuwa anastahiki kushiriki katika Mpango wa Watoto Wachanga, mratibu wa huduma ataongoza kubuniwa kwa mpango wa IFSP.
- Kubuniwa kwa mpango wa kwanza wa IFSP lazima kufanyike ndani ya siku 45 kuanzia siku ya kuelekezwa.

### 5. Utoaji wa Huduma

- Mtoto wako atapokea huduma kama ilivyobainishwa katika mpango wa IFSP.
- Huduma zilizotajwa kwenye mpango wa IFSP zinapaswa kuanza kutolewa ndani ya kipindi cha siku 30 baada ya kubuniwa kwa mpango wa IFSP na kutiwa saini na familia.

> Wazazi wanaweza kuchagua kuendelea kushiriki kwa utaratibu wao, kukomesha utathmini wa hali ya kustahiki kushiriki au kujiondoa kwenye mpango wakati wowote.

### 6. Ukaguzi wa Mpango wa IFSP

- Kadri mahitaji ya mtoto na familia yako yanavyobadilika, misaada na huduma pia zinaweza kuhitaji kubadilika.
- Mpango wa IFSP utakaguliwa angalau kila miezi sita ili kuhakikisha bado unaendana na vipaumbele vyako na mahitaji ya mtoto na familia yako.
- Unaweza kuomba mpango wako wa IFSP usasishwe au ukaguliwe wakati wowote.

**Hatua za Baadaye: Kuondoka katika Mpango**

### 7. Mpito

- Watoto huondoka katika Mpango wa Watoto Wachanga wakati hawastahiki tena kushiriki katika mpango au wanapofikisha umri wa miaka mitatu.
- Mipango ya mpito hubainishwa katika mpango wa IFSP.

# Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina

NC DEPARTMENT OF
**HEALTH AND HUMAN SERVICES**
Division of Child and Family Well-Being
NC Infant-Toddler Program (NC ITP)

Jimbo la North Carolina
Idara ya Afya na Huduma za Binadamu
Sekta ya Ustawi wa Watoto na Familia
Kitengo cha Suluhu za Mapema

www.ncdhhs.gov

www.ncdhhs.gov/division-child-and-family-well-being

www.ncdhhs.gov/itp-beearly

Unaruhusiwa Kutoa Nakala

Aprili 2013 | Julai 2019 | Mei 2022 | Oktoba 2023| Julai 2024

*Idara ya Afya na Huduma za Binadamu haibagui kwa msingi wa asili, rangi, utaifa, jinsia, dini, umri au ulemavu katika ajira au utoaji wa huduma.*